**MATANGAZO YA DOMINICA YA 3 YA PASAKA MWAKA 'B'– 14/04/2024**

1. Waumini mnatangazi kuwa parokia imeanzisha huduma ya kwanza kwa waamini watakaopata matatatizo ya kiafya wakati wa misa siku za Jumapili na siku zingine za matukio makubwa parokiani. Huduma hiyo inatolewa na muuguzi (Nurse) katika chumba kilichoko pembeni mwa kanisa la kuabudu. Hivyo basi, waumini mnaombwa kumsaidia muumini atakayepata changamoto ya kiafya afike mahali pale. Kutakuwa na machela na kiti cha magurudumu nje ya kanisa.

2. Jumamosi tarehe 20 April kutakuwa na mkutano wa Halmashauri ya Walei. Wajumbe wa mkutano ni kamati tendaji jumuiya na wenyeviti wa vyama vya kitume. Wote mnaombwa kufika bila kukosa. Viongozi mnaombwa kuchukua barua za mwaaliko getini.

3. Waumini mnaombwa kutumbukiza bahasha za michango yoyote kwenye masanduku ya sadaka yaliyoko ndani ya kanisa au kupeleka kwa ofisi ya parokia na **SI** kuweka kwenye visanduku nje ya kanisa au kwenye stuli kanisani.

4. Kwa wale ambao wangependa kufunga Ndoa za watu wengi tarehe 14/7/2024 mnaombwa kujiandikisha katika ofisi ya Paroko.

5. Wazazi wa watoto walio Batizwa 01/4/2024 mnaombwa kuchukua vyeti vyenu katika ofisi ya Parokia kuanzia Jumanne.

6. Uongozi wa Uwaka Parokia K/Ndege unawaomba wanaume wote wa Parokia kujiandaa na Mchango maalum tarehe 21/4/2024 kwa ajili ya kuziba upungufu wa deni letu la kituo cha waseminary – Miyuji la 1,606,000/=

7. Mafundisho ya ndoa mwezi huu yatakuwa tarehe **19, 20, na 21.** Wanaotarajia kufunga ndoa mnaombwa kujiandikisha ofisini.

8. Leo mara baada ya Misa ya pili, Masista watawapelekea wagonjwa na wazee Ekaristi Takatifu kwenye Jumuiya zifuatazo **MT. PETER CLAVER, MT. AUGUSTINO, MT. GEMMA GALGAN, MT. MONICA, MT. ANTONY DANIEL, MT. DAVID LEWIS. Jumapili Ijayo wajiandae Jumuiya zifuatazo**: MT. JOSEPHINE BAKITA, MT. YOHANE PAULO WA II, MT. MAXIMILIAN KOLBE, MT. YOHANE WA MSALABA, MT. CLARA WA ASISSI, MT. FRANCIS WA ASISSI. Mama na baba huruma mnaombwa kuwachukua Masista karibu na Sakristia.

9. Gazeti la kiongozi na la kimisionari la Enendeni yanapatikana hapo nje.

10. Viongozi wa Jumuiya mnajulishwa kuwa Karismatiki Katoliki Parokia watafanya Semina Jumuiyani kuhusu Roho Mtakatifu kila Jmosi kuanzia tar 20 April hadi 11 May 2024. Mnaombwa kujiandaa kuwapokea na kuwapa ushirikiano. Ratiba ya Semina inapatikana ubao wa Matangazo.

11. Viongozi wa Jumuiya mnajulisha kuwa Utume wa Fatima umeandaa Novena itakayoanza tareh 16 April hadi 24 April 2024 kila siku, kuanzia saa 9 mpaka 11 jioni. Mkesha utakuwa tarehe 25 April 2024 na utaanza saa moja usiku. Tafadhali wajulishe wanajumuiya wako.

12. Tunashukuru Jumuiya ya **MT. PETER CLAVERY** na **MT. BERNADETHA** kwa kazi nzuri ya usafi na kusimamia utaratibu wa Ibada. Juma lijalo ni zamu ya Jumuiya ya (**A) MT. GABRIEL MALAIKA MKUU** na **(B) MT. JEAN MARIA MUZEEY.** Jumuiya ya **MT. CLARA WA ASISSI** na **MT. MONICA** wajiandae.

**13. NDOA. (SOMA MATANGAZO YA "KWA MARA YA KWANZA TU")**

a) Kwa mara ya **Tatu**: Ndg. **Eliya Ernest**, baba yake ni **Ernest Rutakorezibwa** na mama yake ni **Celestina Kokuramuka** anataka kufunga ndoa na **Mariagoreth Gabriel**, baba yake ni **Gabriel Mayo** na mama yake ni **Aurelia Ignas.** Wote wanasali katika parokia ya **K/Ndege**, **Jimbo Kuu la Dodoma.**

b) Kwa mara ya **Tatu**: Ndg. **Ahazi Leonard**, baba yake ni **Leonard Ngailo** na mama yake ni **Josephina Mahenge** anataka kufunga ndoa na **Winfrida Asheri**, baba yake ni **Asheri Malima** na mama yake ni **Dorice Jeremia.** Wote wanasali katika parokia ya **K/Ndege**, **Jimbo Kuu la Dodoma.**

**14.** Matangazo haya yanapatikana kwenye tovuti ya Parokia: **kndege.or.tz**